# HOTUBA YA MHESHIMIWA WAZIRI MHANDISI ISACK KAMWELWE, WAZIRI WA UCHUKUZI KATIKA KATIKA HAFLA YA UZINDUZI WA MFUMO WA TIKETI ZA KIELEKTRONIKI (e-TICKETING SYSTEM) UNAOFANYIKA TAREHE 4.4.2020

Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Reli : Profesa John Kondoro;

Wajumbe wa Bodi ya Shirika la Reli Tanzania,

Mtendaji Mkuu wa mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA)

Kaimu Mkurugenzi Mkuu TRC – Ndg: Focus Makoye Sahani

- Uongozi wa Shirika la Reli Tanzania ,
- Wafanyakazi TRC,
- Pamoja na Wanahabari,

**Habari za Asubuhi;**

**Wageni waalikwa Mabibi na Mabwana;**

Awali ya yote nianze Kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha sote kuwa hapa leo, kwenye hafla ya kushuhudia uzinduzi wa mfumo wa tiketi wa kielektroniki wa shirika la Reli Tanzania.

**Wageni waalikwa Mabibi na mabwana;**

Wote tunafahamu kuwa TRC ina jukumu kubwa la kutoa huduma za usafirishaji wa abiria na mizigo ndani ya nchi na nje ya nchi. Sambamba na Ujenzi wa reli ya kisasa unaoendelea (SGR) pamoja maboresho ya miundombinu ya reli yanayoendelea kufanyika

nimetaarifiwa kuwa kuna kuongezeka kwa ufanisi kwa kiasi kikubwa katika usafirishaji wa mizigo na abiria kwenda mikoa ya bara hususani Kigoma, Mwanza na Katavi na hivi karibuni Kilimanjaro. Hali hii imechochea wadau wa usafirishaji na wananchi kwa ujumla kutumia huduma zitolewazo na TRC. Nawapongeza sana Bodi, Menejimenti na wafanyakazi wa TRC kwa jitihada zinazoleta tija kwa maslahi ya taifa.

**Wageni waalikwa mabibi na mabwana**

Ni dhahiri kuwa katika uimarishaji wa uendeshaji wa Shirika la Reli Tanzania matumizi ya teknolojia ni muhimu sana ili kupunguza matumizi, kuongeza ufanisi na kuongeza mapato. Serikali kwa upande wake imekuwa ikielekeza TRC kuhusu umuhimu wa matumizi ya teknolojia ili kuboresha huduma zake na kuongeza ufanisi hasa katika ukusanyaji wa mapato yake kielektroniki.

**Wageni waalikwa Mabibi na mabwana**

TRC kama ilivyo kwa mashirika mengine mengi ya umma yanayofanya biashara na kukusanya mapato yamekuwa na changamoto nyingi za ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mifumo ambayo haitumii teknolojia na hiyvo kupoteza mapato kutokana na vitendo vya baadhi ya wafanyakazi wasio waaminifu.

Serikali ya Awamu ya Tano, chini ya Uongozi wa Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, ilitambua

changamoto hiyo, na hivyo kuziagiza taasisi zote za serikali zinazo kusanya mapato kuhakikisha kuwa wanatumia mifumo ya kielektroniki katika kukusanya mapato yake.

**Wageni waalikwa Mabibi na mabwana**

Shirika la Reli Tanzania kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) wametekeleza agizo hilo na wametengeneza mfumo wa Tiketi wa kielectroniki (e-Ticket) na Usimamizi wa Mizigo kwa njia ya Mtandao (e-Cargo) na tumekusanyika leo kushuhudia uzinduzi wake rasmi. Mfumo huu umeiwezesha TRC kuimarisha ukusanyaji mapato yake na kuondoa kabisa matumizi ya tiketi za kuandika kwa mkono.

Kwa Mwaka 2017/18 kabla ya matumizi ya mfumo wa Kielektroniki wa tiketi inaonyesha kuwa TRC ilikusanya mapato ya sh 39.7 bilioni na baada ya kuanza kwa matumizi ya mfumo huu mapato yaliongezeka na kufikia kiasi cha shilingi 44.7 bilioni kwa mwaka 2018/19.

Hivyo napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza sana TRC na eGA kwa kazi hiyo nzuri.

**Wageni waalikwa Mabibi na mabwana**

Serikali ya awamu ya Tano imekuwa ikiwekeza fedha kuimarisha sekta ya miuondombinu ya reli nchini kwa ujenzi wa reli ya kisasa – SGR, kuboresha reli ya kati *Meter Gauge Railway* (MGR) kati ya Dar es Salaam na Isaka, kufanya ukarabati wa njia ya reli za Tanga hadi

Arusha ambayo ilikuwa hazifanyi kazi kwa zaidi ya miaka 20 na kuifungua.

Kuimarika huko kwa njia za reli kumefungua fursa mpya kwa shirika kuongeza ufanisi katika biashara zake za abiria na mizigo na hivyo basi kuwepo kwa mifumo dhabiti ya ukusanyaji wa mapato unahakikisha shirika litaweza kujiendesha na kuanza rejesha gawio kwa serikali kwa uwekezaji huu mkubwa.

Matokeo ya uwekezaji huu umefanya idadi ya shehena za mizigo imeongezeka kutoka tani 186,963 mwaka 2016 hadi kufikia tani 399,784 mwaka 2019. Pia idadi ya abiria imeongezeka kutoka abiria 411,172 mwaka 2015 hadi abiria 578,439 mwaka 2019.

**Wageni waalikwa Mabibi na mabwana**

Pamoja na mfumo huu kusaidia kupunguza upotevu wa mapato, mfumo una faida zingine kadhaa zikiwemo

i. Kuboresha huduma kwa kurahisisha upatikanaji wa tiketi kwa kuwezesha wateja kununua tiketi kupitia mtandao wa intaneti na hivyo kupunguza ulazima wa wateja kufika stesheni ili waweze kupata tiketi.

ii. Kupunguza gharama za mauzo kwa kuondoa gharama za utengenezaji wa vitabu vya tiketi za kuandika kwa mkono.

iii. Mfumo umerahisisha upatikanaji wa taarifa mbalimbali zinazohusiana na usafirishaji wa abiria na mizigo na hivyo kuwezesha shirika kupanga mipango yake kwa uweledi zaidi.

iv. Kwa mfumo kutengenezwa kwa kutumia wataalamu wazawa walio katika taasisi za serikali yaani eGa na TRC kumeokoa fedha nyingi. Pia uzoefu uliopatikana kwa kutengeneza mfumo huu unaweza kutumika katika sekta na mashirika mengine ya usafirishaji ya umma kwa gharama nafuu.

**Wageni waalikwa Mabibi na mabwana**

Katika kuendeleza kuunga mkono juhudi zinazofanywa na Mh.Rais Dokta John Pombe Magufuli kulifufua shirika la Reli Tanzania naomba kuchukua nafasi hii kuwahimiza watanzania wote kutumia huduma zilizoboreshwa za kusafirisha mizigo yao kwa treni na pia kutumia usafiri wa treni za abiria kuelekea sehemu mbalimbali nchini. Pia niwahimize watumie fursa zilizomo katika mfumo huu wa tiketi wa kielectroniki kwa kukata tiketi kwa kutumia mtandao na kulipa kwa wao wenyewe kwa mtandao.

**Wageni waalikwa mabibi na mabwana**

Mwisho kabisa napenda kuwashukuru tena eGA kwa kushirikiana na TRC katika kufanikisha utengenezaji wa mfumo huu wa tiketi. Pia nawaomba waendeleze ushirikiano huo katika kutengeneza mifumo mingine zaidi ambayo itaboresha utendaji kazi wa shirika. Jambo hili

limeonyesha kuwa watanzania tukiamua tunaweza kufanya mambo makubwa sana bila kuwategemea wafadhili au mataifa mengine.

Baada ya kusema haya sasa niko tayari kuzindua mfumo wa tiketi za kielektroniki (e-ticketing system) wa shirika la Reli Tanzania

Asanteni sana kwa kunisikiliza.

**Reli Yetu, Maendeleo Yetu, Taifa letu, Hapa Kazi Tu.**